

HALMASHAURI YA WILAYA YA URAMBO

BAJETI YA MAPATO NA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2017/2018.

SURA YA KWANZA.

MIONGOZO MBALIMBALI ILIYOTUMIKA KUANDAA MPANGO NA BAJETI.

1.0: DIRA NA DHAMIRA YA HALMASHAURI YA WILAYA YA URAMBO

1.1: Dira ya Halmashauri ya Wilaya:

“Kuwa na maendeleo endelevu ya Kijamii na Kiuchumi kwa wananchi wa Wilaya ya Urambo.”

1.2: Dhamira/Mwelekeo/Taswira:

“Kuweka mazingira ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa watu wote kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika kutoa huduma bora na kwa wakati kwa kutumia rasilimali zilizopo”.

2.0: Majukumu ya Halmashauri ya Wilaya ni haya yafuatayo:-

2.1.1: Kudumisha na kuimarisha amani na Utawala bora na wa kisheria.

2.1.2: Kuboresha uchumi na maendeleo ya jamii

2.1.3: Kutunga sheria ndogo ndogo za kusimamia utekelezaji wa maamuzi ya Halmashauri.

2.1.4: Kupunguza na kuzuia Matukio ya makosa ya jinai na kulinda mali za wananchi zilizopatikana kihalali.

2.1.5: Kuinua na kuendeleza kilimo na Mifugo.

2.1.6: Kupunguza umaskini kwa kutoa msaada kwa vijana na wasiojiweza.

2.1.7: kupiga vita umaskini, magonjwa na ujinga.

2.2.0: Madhumuni makuu ya Halmashauri ya Wilaya:

Kwa kuzingatia Dira, na Mwelekeo/Taswira ya Halmashauri, kuna maeneo makuu ambayo yamekuwa ni msingi wa kutekeleza majukumu yaliyoainishwa katika sheria iliyounda Halmashauri kama ifuatavyo:-

2.2.1: Kuongeza ushiriki wa wadau na jamii katika mchakato wa kupanga na kutekeleza mipango ya maendeleo.

2.2.2: Kuongeza fursa za upatikanaji wa huduma za Elimu.

2.2.3: Kuendeleza ubora wa Afya na upatikanaji wa huduma zake.

2.2.4: Kuanzisha, kuendeleza na kuhifadhi Maliasili na vyanzo vya Maji.

2.2.5: Kuchangia katika kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara na kuinua kipato na hifadhi ya chakula.

2.2.6: Kuendeleza njia za mawasiliano na usafirishaji, kusimamia ukuaji wa miji na matumizi bora ya ardhi hadi vijijini.

2.2.7: Kuwajengea uwezo wafanyakazi na kuhakikisha upatikanaji wa vitendea kazi pamoja na kuimarisha Utawala bora.

Mpango na Bajeti ya Halmashauri kwa mwaka 2017/2018 vimeandaliwa kwa kuzingatia sheria ya fedha ya Serikali za Mitaa Na. 9 ya mwaka 1982 kifungu cha 43 (1) na kuzingatia mfumo wa matumizi ya muda wa kati (Medium Term Expenditure Framework), mwongozo ulitolewa na Wizara ya Fedha .Pamoja na maelekezo mengine yaliyotolewa na Serikali kuu na vipaumbele vya Halmashauri ya Wilaya.

Makisio haya yanahusu mapato ya ndani ya Halmashauri, ruzuku ya mishahara na matumizi mengineyo toka Serikali Kuu, ruzuku ya miradi ya maendeleo kutoka Serikali Kuu na wafadhili wengineo.

3. MALENGO YA BAJETI YA MWAKA 2017/2018

Katika kuandaa bajeti ya mwaka wa Fedha 2017/2018, Halmashauri imeendelea kuzingatia malengo mbalimbali kama yalivyobainishwa;

- Kuendelea kujenga uwezo wa kiutawala katika ngazi zote za kiutawala, Wilayani hadi Vijijini.
- Kupeleka asilimia 20% ya mapato ya ndani kwenye vijiji na kata kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo
- Kuchangia 10% katika mifuko ya vijana na wanawake.
- Kuendelea kuboresha utunzaji wa takwimu na kuimarisha mfumo wa utoaji habari kwa Serikali za Vijiji, Kata na Wadau wengine.
- Kuendelea kuboresha mfumo wa mawasiliano na miundo mbinu kwa kuongeza na kuimarisha mtandao wa barabara hasa za vijijini.
- Kuboresha muundo wa Halmashauri na kuboresha utendaji wa kazi.
- Kuimarisha ufuatiliaji na utekelezaji wa miradi ya maendeleo na shughuli zingine katika jamii.
- Kuiwezesha jamii kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo.
- Kuimarisha Demokrasia na Utawala bora kwa kuhakikisha uchaguzi Mdogo wa Serikali za mitaa unafanyika kila inapobidi.
- Kuboresha na kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za jamii.

4. UIMARISHAJI WA UKUSANYAJI WA MAPATO YA NDANI

Halmashauri itaendelea kutumia mfuko wa pembejeo pamoja na uboreshaji wa vyama vya Ushirika ili kuunga mkono wakulima katika kukuza na kuboresha kilimo cha tumbaku ambacho kinaipatia Halmashauri na wananchi wake pato kubwa. Aidha hamasa kwa mazao mengine itaendelea kupewa umuhimu ili kuongeza pato la mwananchi wa Urambo,

Mwisho Halmashauri itaendelea kuboresha njia ya ukusanyaji wa mapato kwa kutumia njia ya kielektroniki.

5. MWONGOZO WA UANDAAJI WA BAJETI NA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2017/2018

Mwongozo uliotolewa na Wizara ya Fedha , umelenga katika kuandaa bajeti ya kipindi cha 2017/2018 – 2021/2022 kwa ufanisi .Katika mwongozo huo, imeelezwa bayana kuwa Tanzania inatekeleza mkakati wa kitaifa wa kukuza uchumi na

kupunguza umaskini (MKUKUTA) na kwamba Serikali za Mitaa ni wadau muhimu katika utekelezaji wa mpango huu.

Mwongozo huo unazitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa kuzingatia maeneo yaliyopewa kipaumbele yatakayoivezesha kukua kiuchumi na kupunguza umaskini. Kwa mantiki hiyo Mpango na Bajeti wa Halmashauri umezingatia masuala yafuatayo:-

- i. Kujenga uwezo wa Halmashauri katika kuandaa mipango,utekelezaji wa mipango,usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo katika kutoa Huduma kwa jamii
- ii. Kusimamia amani na utii wa sheria kwa wananchi
- iii. Kuboresha mazingira bora kwa ajili ya kuongeza uwekezaji.
- iv. Kuboresha usimamizi wa fedha na mali za umma.
- v. Kuboresha ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri yatokanayo na vyanzo vya ndani.
- vi. Usimamiaji na utekelezaji wa Kilimo katika uongezaji wa ubora wa mazao, utunzaji na masoko.
- vii. Kuweka kipaumbele katika Kutekeleza miradi iliyo katika mpango wa matokeo makubwa sasa (BRN).

6. MAAGIZO YA SERIKALI NA MAAMUZI YA HALMASHAURI.

Bajeti ya Halmashauri ya Wilaya imezingatia maelekezo/maagizo mbalimbali ya Serikali na maamuzi ya Halmashauri kama ifuatavyo:

6.1. Maagizo ya Serikali

- a) Kupeleka 20% ya mapato ya ndani katika vijiji na kata.
- b) Kuchangia Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa (LGLB).
- c) Kutenga fedha kwa ajili ya mafunzo ya watumishi ili kuongeza tija.
- d) Ulipaji wa madeni ya Watumishi, Wazabuni na Wakandarasi.
- e) Kutekeleza dhana nzima ya kilimo kwanza katika kuhakikisha kuwa kuna chakula cha kutosha pamoja na kumwongezea mwananchi kipato.

- f) Kuimarisha mamlaka za Serikali za Mitaa zilizo ndani ya Halmashauri ya Wilaya yaani Mamlaka ya Mji Mdogo Urambo na Serikali za Vijiji.
- g) Kutofanya manunuzi ya magari, isipokuwa kwa kupata kibali kutoka ofisi ya Waziri mkuu.
- h) Utekelezaji wa maagizo ya Hombolo.
- i) Utekelezaji wa maagizo ya kamati ya Bunge ya hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) yaliyotolewa katika kikao cha kujadilia hesabu za Halmashauri ya Wilaya ya Urambo za mwaka 2014/2015 mjini Dodoma, ambapo iliagizwa Halmashauri kupeleka 5% ya mapato yake ya ndani katika vikundi vya Vijana na 5% Katika vikundi vya akina mama pamoja na kulipa madeni ya miaka ya nyuma ili kukidhi mahitaji ya kisheria katika kuchangia mifuko hii.

6.2. Maamuzi ya Halmashauri:

- a. Kutoa kipaumbele katika kukamilisha miradi viporo.
- b. Kupeleka 20% ya mapato ya ndani kwenye vijiji na kata kwa ajili ya shughuli za maendeleo ambapo kila kijiji na kila kata vitapewa Tsh.7,044,415.58
- c. Kusaidia watoto wasiojiweza wanaosoma shule za sekondari kidato cha tano na sita kwa kuwalipia karo.
- d. Kuwekeza katika maeneo yatakayosaidia kuongeza mapato ya Halmashauri kama vile;- Stendi ya kudumu, Masoko na Minada.
- e. Kuchangia ujenzi wa shule za sekondari za wananchi.
- f. Kuchangia miradi ya wahisani.
- g. Kutenga fedha za mikopo kwa ajili ya akina mama 5% na vijana 5% kutoka mapato ya ndani.
- h. Kutoa mafunzo kwa watumishi na waheshimiwa madiwani.
- i. Kuimarisha ukusanyaji wa mapato katika vyanzo vya mapato ambavyo vimekuwa havikusanywi kikamilifu.

SURA YA PILI

MAPITIO YA BAJETI NA MPANGO WA MAENDELEO WA MWAKA 2015/2016.

1.1 MAPATO

Katika mwaka wa fedha wa 2015/2016 Halmashauri ya Wilaya ya Urambo ilikisia kukusanya jumla ya Tshs **19,082,371,200.00** kutokana na vyanzo vifuatavyo:-

(a).Mapato ya Ndani

Jumla ya Tsh. **2,649,569,000.00** zilipangwa kukusanywa kutoka mapato ya ndani kupitia vyanzo mbalimbali vya Halmashauri.

(b).Ruzuku toka Serikali kuu

Ruzuku iliyotengwa na Serikali kwa matumizi ya Idara zinazopata ruzuku pamoja na Miradi ya Maendeleo ni kama ifuatavyo;

(i). Ruzuku ya mishahara na matumizi mengineyo:-

Mishahara 11,904,868,000.00

Matumizi mengineyo 1,309,033,000.00

Jumla ndogo 13,213,901,000.00

(ii). Ruzuku ya mifuko ya pamoja na Miradi ya maendeleo

<u>MRADI</u>	<u>FEDHA ZA WAFADHILI</u>	<u>FEDHA ZA NDANI</u>	<u>JUMLA</u>
HSBF-Urambo	371,350,000.00	0	371,350,000.00
Road fund	0	743,210,000.00	743,210,000.00
HIV/AIDS	12,479,000.00	0	12,479,000.00
LGSP- CDG	0	715,329,000.00	715,329,000.00
Livestock Development Fund	0	10,415,000.00	10,415,000.00
RWSSP-(CDG)	43,377,000.00	0	43,377,000.00
SEDP-World Bank	27,957,000.00	0	27,957,000.00
DIDF	82,750,000.00	0	82,750,000.00
Mfuko wa Jimbo	0	44,865,000.00	44,865,000.00
Jumla ndogo	537,913,000.00	1,513,819,000.00	2,051,732,000.00

c. Wafadhili wasiopitisha fedha zao Hazina na michango ya jamii.

512A	Land Administration-User Fee	50,000,000.00
508F	CHF	41,520,000.00
508F	NHIF	47,000,000.00
508F	PMTCT	148,288,500.00
508F	CTC	135,969,100.00
508F	HBC	26,168,650.00
508F	MCH/RCH	67,097,950.00

509B	Secondary operations fees	150,170,000.00
507B	EQUIP	500,955,000.00
	Jumla ndogo	1,167,169,200.00
Jumla kuu		19,082,371,200.00

d. Makusanyo.

Hadi kufikia mwezi Juni 2016 Halmashauri imekwisha kusanya Jumla ya Tshs. **22,187,161,050.75** kwa ajili ya shughuli mbalimbali za mapato ya ndani, ruzuku na miradi ya maendeleo kwa mchanganuo ufuatao;-

S/N	Maelezo	Kiasi kilichopangwa.	Kiasi kilichokwisha kusanywa/pokelewa	Asilimia
1	Mapato ya ndani	2,649,569,000.00	2,239,548,542.67	84.5
2	Ruzuku toka serikali kuu-OC	1,309,033,000.00	861,598,740.00	65.8
3	Ruzuku toka serikali kuu-Mishahara	11,904,868,000.00	15,508,628,410.09	130.3
4	Miradi ya maendeleo na Wafadhili wengine	3,218,901,200.00	3,577,385,257.99	111.1
	Jumla	19,082,371,200.00	22,187,161,050.75	

Fedha ya miradi inaonekana kuletwa kiasi kikubwa kutokana na Fedha ya TASAF Tsh.1,136,641,500.00 na DIDF Tsh.331,000,000 kutokuwemo kwenye makisio ya mwaka 2015/2016

2.0.MATUMIZI

Hadi Juni 2016 Halmashauri imekwishatumia kiasi cha **Tsh.21,708,294,130.80** kwa mchanganuo ufuatao:-

S/N	Maelezo	Kiasi kilichotumika
1	Mapato ya ndani	891,716,464.39
2	Ruzuku toka serikali kuu-OC	902,090,786.91
3	Ruzuku toka serikali kuu-Mishahara	15,508,628,410.09
4	Miradi ya maendeleo na Wafadhili wengine	4,405,858,469.41
	Jumla	21,708,294,130.80

SURA YA TATU.

MAPITIO YA BAJETI NA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2016/2017 HADI DESEMBA, 2016.

1.1 MAPATO

Katika mwaka wa fedha wa 2016/2017 Halmashauri ya Wilaya ya Urambo ilikisia kukusanya jumla ya **Tshs 25,504,627,310.00** kutokana na vyanzo vifuatavyo:-

(a)Mapato ya Ndani.

Kiasi cha Tsh **2,667,761,000.00** kilitarajiwa kukusanywa kutoka mapato ya ndani.

(b)Ruzuku ya Mishahara na matumizi mengineyo

Ruzuku iliyotengwa na Serikali kwa matumizi ya Idara zinazopata ruzuku kwa ajili ya mishahara na matumizi mengineyo ni kama ifuatavyo;

i. Mishahara	16,083,801,000.00
ii. Matumizi mengineyo	<u>1,161,273,000.00</u>

Jumla ndogo **17,245,074,000.00**

(c).Ruzuku ya mifuko ya pamoja na Miradi ya maendeleo

<u>MRADI</u>	<u>FEDHA ZA WAFADHILI</u>	<u>FEDHA ZA NDANI</u>	<u>JUMLA</u>
HSBF-Urambo	547,553,000.00	0	547,553,000.00
ROAD FUND	0	743,210,000.00	743,210,000.00
LGSP- CDG	0	693,842,000.00	693,842,000.00
RWSSP-CDG	157,317,000.00	0	157,317,000.00
SEDP-WORLD BANK	111,828,000.00	0	111,828,000.00
SPHC for Results	1,177,929,810.00	0	1,177,929,810.00
MFUKO WA JIMBO	0	44,865,000.00	44,865,000.00
Jumla miradi	1,994,627,810.00	1,481,917,000.00	3,476,544,810.00

d. Wafadhili wasiopitisha fedha zao hazina

508B	EGPAF-PMTCT	141,400,000.00
508B	EGPAF-CTC	131,325,000.00
508B	CHF	68,040,000.00
508B	NHIF	98,000,000.00
507B	EQUIP	550,252,500.00
509B	School fees-'A'Level	27,230,000.00
508B	USER FEE-HOSPITAL	100,000,000.00
527B	TASAF	999,000,000.00
	Jumla ndogo	2,115,247,500.00
Jumla kuu		25,504,627,310.00

d. Makusanyo.

Hadi kufikia mwezi Desemba, 2016 Halmashauri imekwisha kusanya Jumla ya Tshs.**10,657,913,796.61** kwa ajili ya shughuli mbalimbali za mapato ya ndani, ruzuku na miradi ya maendeleo kwa mchanganuo ufuatao;-

S/N	Maelezo	Kiasi kilichopangwa.	Kiasi kilichokwisha kusanywa/pokelewa	Asilimia
1	Mapato ya ndani	2,667,761,000.00	1,546,657,295.15	57.9
2	Ruzuku toka serikali kuu-OC	1,161,273,000.00	287,652,068.00	24.8
3	Ruzuku toka serikali kuu-Mishahara	16,083,801,000.00	7,176,092,610.00	44.6
4	Miradi ya maendeleo na Wafadhili wengine	5,591,792,310.00	1,647,511,823.46	29.5
	Jumla	25,504,627,310.00	10,657,913,796.61	42

Makusanyo haya yanaonyesha kuwa bado kuna changamoto ya kuchelewa kuletewa fedha za ruzuku toka serikali kuu na hasa fedha za miradi ya maendeleo na matumizi mengineyo-oc.

2.0.MATUMIZI

Hadi Desemba,2016 Halmashauri imekwishatumia kiasi cha **Tsh.10,374,655,132.65** kwa mchanganuo ufuatao:-

S/N	Maelezo	Kiasi kilichokwisha kusanywa/pokelewa	Kiasi kilichotumika
1	Mapato ya ndani	1,546,657,295.15	1,306,078,985.34
2	Ruzuku toka serikali kuu-OC	287,652,068.00	289,642,854.98
3	Ruzuku toka serikali kuu-Mishahara	7,176,092,610.00	7,176,092,610.00
4	Miradi ya maendeleo na Wafadhili wengine	1,647,511,823.46	1,602,840,682.33
	Jumla	10,657,913,796.61	10,374,655,132.65

SURA YA NNE.

BAJETI NA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2017/2018

1.1 MAPATO

Katika mwaka wa fedha wa 2017/2018 Halmashauri ya Wilaya ya Urambo inakisia kukusanya jumla ya **Tsh.23,543,222,810.00** kutokana na vyanzo vifuatavyo:-

(a)Mapato ya Ndani.

Kiasi cha Tsh **2,696,942,000.00** kinatarajiwa kukusanywa kutoka mapato ya ndani.

(b)Ruzuku ya Mishahara na matumizi mengineyo

Ruzuku iliyotengwa na Serikali kwa matumizi ya Idara zinazopata ruzuku kwa ajili ya mishahara na matumizi mengineyo ni kama ifuatavyo;

i. Mishahara	14,396,041,000.00
ii.Matumizi mengineyo	<u>770,612,000.00</u>

Jumla ndogo **15,166,653,000.00**

(c).Ruzuku ya mifuko ya pamoja na Miradi ya maendeleo

<u>MRADI</u>	<u>FEDHA ZA WAFADHILI</u>	<u>FEDHA ZA NDANI</u>	<u>JUMLA</u>
HSBF-Urambo	509,198,000.00	0	509,198,000.00
ROAD FUND	0	939,330,000.00	939,330,000.00
LGDG	0	1,200,205,000.00	1,200,205,000.00
RWSSP	465,389,000.00	0	465,389,000.00
SEDP-WORLD BANK	111,828,000.00	0	111,828,000.00
MFUKO WA JIMBO	0	52,768,000.00	52,768,000.00
ELIMU BURE-MSINGI	0	462,921,000.00	462,921,000.00
ELIMU BURE-SEKONDARI	0	305,168,000.00	305,168,000.00
Jumla miradi	1,086,415,000.00	2,960,392,000.00	4,046,807,000.00

d. Wafadhili wasiopitisha fedha zao hazina

508B	EGPAF-PMTCT	141,400,000.00
508B	EGPAF-CTC	131,325,000.00
508B	CHF	153,035,810.00
508B	NHIF	98,000,000.00
509B	School fees-'A'Level	25,060,000.00
508B	USER FEE-HOSPITAL	85,000,000.00
527B	TASAF	999,000,000.00
	Jumla ndogo	1,632,820,810.00
Jumla kuu		23,543,222,810.00

2.0. MAELEZO KUHUSU MAPATO NA MATUMIZI YA MAPATO YA NDANI (OWN SOURCE) KWA MWAKA 2017/2018

Halmashauri imejiwekea Mkakati wa kuhakikisha kuwa mapato yote ya ndani yanakusanywa na kufikia malengo ya Jumla ya Tshs **2,696,942,000.00**

Njia ambayo itatusaidia ni kukusanya kwa kutumia mtandao, Pia vizuizi vya ukaguzi katika maeneo mbalimbali vitawekwa ili kuhakiki ulipaji wa kodi mbalimbali bila kuleta usumbufu kwa wakulima na wafanyabiashara wanaotimiza wajibu wao kwa kulipa kodi ipasavyo.

Mchanganuo wa vyanzo vya mapato umeambatanishwa kama kiambatanisho A.

3.0 MATUMIZI YA FEDHA YA MAPATO YA NDANI.

A. Miradi ya maendeleo

Kiasi cha Tshs **1,618,165,000.00** kinachotokana na mapato ya ndani ya Halmashauri kimetengwa kwa ajili ya kuchangia katika shughuli mbalimbali za maendeleo nje ya matumizi ya kawaida katika Idara za Halmashauri ya Wilaya.

Mchanganuo wake ni kama ifuatavyo:

<u>Na</u>	<u>Maelezo</u>	<u>Tshs</u>
1	Miradi ya maendeleo-wilaya	757,610,800.00
2	Miradi ya maendeleo-vijiji	542,420,000.00
3	Mfuko wa wanawake	134,847,100.00
4	Mfuko wa vijana	134,847,100.00
5	Michango mbalimbali	48,440,000.00
	<u>Jumla</u>	<u>1,618,165,000.00</u>

B. Uendeshaji wa vikao vya Halmashauri na posho mbalimbali za viongozi

Jumla ya **Tsh.440,438,000.00** zitatumika kwa ajili ya **vikao na posho** mbalimbali za viongozi na zimechanganuliwa kwa kina katika sehemu maalum ('Section'.500C-Civic Expenses).

Aidha mchanganuo wake umeambatanishwa Kama kiambatanisho B,C na E

C. Matumizi ya kawaida na mishahara kwa fedha ya mapato ya ndani katika idara mbalimbali.

Jumla ya matumizi ya kawaida kwa fedha ya mapato ya ndani katika idara mbalimbali ni **Tsh.509,754,000.00** wakati **Tsh. 128,585,000.00** zimetengwa kwa ajili ya mishahara.

D. Uwiano wa matumizi mbalimbali kwa kutumia mapato ya ndani.
Fedha ya mapato ya ndani inapendekezwa kutumika kwa mchanganuo ufuatao;-

S/N	MAELEZO	KIASI KILICHOTENGWA	ASILIMIA YA MAPATO YOTE
1	Miradi ya maendeleo	1,618,165,000.00	60 %
2	Uendeshaji wa vikao na posho za viongozi	440,438,000.00	16.3%
3	Matumizi ya idara mbalimbali	509,754,000.00	18.9%
4	Mishahara	128,585,000.00	4.8 %
	JUMLA	2,696,942,000.00	100%

4.0 MATUMIZI YA RUZUKU TOKA SERIKALI KUU.

Fedha ya ruzuku imepangwa kutumika kama ifuatavyo;-

(a)Ruzuku ya Mishahara na matumizi mengineyo

Matumizi ya Idara zinazopata ruzuku kwa ajili ya mishahara na matumizi mengineyo ni kama ifuatavyo;

i. Mishahara 14,396,041,000.00

ii. Matumizi mengineyo 770,612,000.00

Jumla ndogo 15,166,653,000.00

(b).Ruzuku ya mifuko ya pamoja na Miradi ya maendeleo

MRADI	FEDHA ZA WAFADHILI	FEDHA ZA NDANI	JUMLA
HSBF-Urambo	509,198,000.00	0	509,198,000.00
ROAD FUND	0	939,330,000.00	939,330,000.00
LGDG	0	1,200,205,000.00	1,200,205,000.00
RWSSP	465,389,000.00	0	465,389,000.00
SEDP-WORLD BANK	111,828,000.00	0	111,828,000.00
MFUKO WA JIMBO	0	52,768,000.00	52,768,000.00
ELIMU BURE-MSINGI	0	462,921,000.00	462,921,000.00
ELIMU BURE-SEKONDARI	0	305,168,000.00	305,168,000.00
Jumla miradi	1,086,415,000.00	2,960,392,000.00	4,046,807,000.00

c. Wafadhili wasiopitisha fedha zao hazina na michango ya jamii.

Fedha ya wafadhili wengineo na michango ya jamii imepangwa kutumika kama ifuatavyo;-

508B	EGPAF-PMTCT	141,400,000.00
508B	EGPAF-CTC	131,325,000.00
508B	CHF	153,035,810.00
508B	NHIF	98,000,000.00
509B	School fees-'A'Level	25,060,000.00
508B	USER FEE-HOSPITAL	85,000,000.00
527B	TASAF	999,000,000.00
	Jumla ndogo	1,632,820,810.00
Jumla kuu		23,543,222,810.00